THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL

# Gredi ya 7

# Mwongozo wa Kutathminia

## SEHEMU B na C

## SEPTEMBA 2024

**ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA**

1. Masurufu, kukuza mchicha, kufuga sungura na kuku

**1x1 =1**

2. C **1x1=1**
3. Mtu akilala tajiri na kuamka maskini:
   i. Atashtuka
   ii. Atakata tamaa
   iii. Ataomba masaada kwa marafiki
   iv. Ataomba mkopo
   v. Ataaibika
   vi. Atajuta
   vii. Atajilaumu

**1 x1 =1**

**Tanbihi: Hakiki majibu ya mwanafunzi ipasavyo.**

4. Masurufu- pesa anazopewa mtu kwa ajili ya matumizi ,kwa mfano ya safarini

**1 x1 =1**

5. Hali ya amani/ utulivu/ shwari/ kuthaminiana **1x1 = 1**
6. **Mchwa ni mlezi mwema kwa kuwa:** **1x1 =1**
   i. Anaposhuku kwamba pana hatari anawawazia watoto wake kwanza.
   ii. Anaenda kuwatazama watoto wake chumbani.
7. **Uharibifu wa wadudu kwa ndege:** **1 x 1= 1**
   i. Kuharibu samani k.m mchwa
   ii. Kuwang'ata k.m nyuki
   iii. Kuharibu mimea kama nzige
   iv. Kueneza magonjwa.
8. **Funzo kutokana ana aya ya mwisho:** **1x1 =1**
   i. Ni muhimu kutatua mizozo kwa njia ya amani
   ii. Makao ni muhimu kwa usalama
   iii. Ushirikiano huboresha hali ya Maisha

**UFUPISHO**

9. Mwanafunzi aaandike sentensi inayojumuisha habari kuu zifuatazo : **1x1= 1**
   i. Ulanguzi wa binadamu huhusu kuwauza watu .
   ii. Husababishwa na hali kama vile umaskini.

Mfano. Ulanguzi wa binadamu ni tendo la kuwauza watu na husababishwa na hali kama vile umaskini.

10. Ufupisho wa madhara ya ulanguzi

i. Ulanguzi wa binadamu husababisha utengano, dhiki za kisaikolojia na dhuluma.

**1x1= 1**

11. Ujumbe wa **aya ya mwisho:** **1 x1=1**

i. Kukabiliana na ulanguzi wa binadamu kunatuhitaji tumakinike kuwatambua washukiwa na kuishi kwenye mazingira salama..

12. Kauli, *Hatuna budi* kwa neno moja:

i. sharti/ inatulazimu/ inatupasa/ lazima/ inatubidi

**1x1= 1**

**ZOEZI 4: SARUFI**

13. C (alama 1)

14. A (alama 1)

15. D (alama 1)

16. B (alama 1)

17. C (alama 1)

18. ukali (alama 1)

19. zi-tu (alama 1)

20. Malombe alikuwa akiwatunza ng’ombe wake

Malombe amewahi kuniuzia n’gombe

Malombe angali anawatunza ng’ombe wake

***Hakiki majibu ipasavyo*** (alama 1)

21. Sewe akifanya utafiti mtandaoni ataandika makala bora zaidi

Sewe atakapofanya utafiti mtandaoni ataandika makala bora zaidi

Sewe atafanya utafiti mtandaoni ili aandike makala bora zaidi.

(alama 2)

22. B (alama 1)

23. Taarifa hiyo haikufurahisha (alama 1)

24. Mlezi wangu aliniomba nisome kifungu hicho kwa sauti (alama 2)

25. Maria ametunga hadithi ilhali Joshua amechora picha (alama 2)

26. Mwimbaji alicheza goma hilo vyema. (alama 1)

Goma hilo lilitoa sauti ya kupendeza.

27. Mwenyeji (alama 1)

28. **ZOEZI 5: KUANDIKA**

Hii ni barua ya kirafiki.

1. Iwe na sehemu mbili kuu : Maudhui na muundo
2. Maudhui –umuhimu wa uhifadhi wa maliasili uzingatiwe/ umuhimu wa kuhudhuria hafla. Baadhi ya hoja ni :
    - Kuhakikisha kujitosheleza kwa chakula
    - Maliasili ikichafuliwa magonjwa yanaweza kuzuka na kusambaa
    - Maliasili kama vile misitu, fuo na nyika ni kivutio cha watalii.
    - Ni muhimu kuihifadhi ili kuvirithisha vizazi vijavyo
    - Barua idokeze vile anayehudhuria atafaidika.
    - Anaweza kutaja walialikwa.
    - Anaweza kumwelekeza mahali pa hafla tarehe na wakati

3. **Muundo**

Muundo wa barua ya kirafiki uzingatiwe

- Anwani ya mwandishi iandikwe upande wa kulia.
- Tarehe
- Mtajo/ Kongowezi
- Utangulizi – kiini cha hafla- uhifadhi wa maliasili
- Mwili- Hoja kuu zijadiliwe katika aya.
- Mfuatano ufaao wa hoja uzingatiwe.
- Mtindo- Lugha ya barua ya kirafiki izingatiwe
- Hitimisho- ajumuishe hoja zake huku akisisitiza kiini cha mwaliko/hafla

4. Mwanafunzi azingatie sura ya
    i. Barua ya kirafiki iwe na anwani ya mwandishi upande wa kulia wa karatasi.

**Tanbihi:**
    i. Mwanafunzi ana uhuru wa kuzingatia masuala yoyote yanayohusiana na maudhui ya insha lengwa.

ii. Katika kutuza, mwalimu azingatie vigezo vifuatavyo ili kutathmini kiwango cha utendaji cha mwanafunzi. Viwango hivyo ni Kiwango cha 4, 3,2 na 1
iii. Kiwango hicho ndicho atakachorekodi kwenye jedwali la alama.

**Viwango vya kutathmini**

| **Vigezo vya kutathmini** | **4**<br><br>**Kuzidi matarajio** | **3**<br><br>**Kufikia matarajio** | **2**<br><br>**Kukaribia matarajio** | **1**<br><br>**Mbali na matarajio** |
|---|---|---|---|---|
| Sarufi na ufundi wa uandishi | Anadhihirisha umilisi wa kiwango cha juu cha sarufi, uakifishaji na uendelezaji wa maneno katika uandishi wake. | Anatumia sarufi, alama za uakifishaji na kuendeleza maneno ipasavyo katika uandishi.<br><br>Hata hivyo, ana makosa machache ambayo hayatatizi usomaji. | Ana makosa ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno ambayo yanatatiza usomaji wa sehemu za insha yake. | Ana makosa mengi ya sarufi, uakifishaji na maendelezo ya maneno kuanzia mwanzo hadi mwisho wa uandishi.<br><br>Msomaji anaweza tu kukisia maana. |
| Mwandiko | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br><br>Anatenganisha herufi zote ipasavyo kwenye mistari.<br><br>Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno kutoka mwanzo hadi mwisho wa insha. | Ana mwandiko nadhifu unaosomeka kwa urahisi.<br><br>Anatenganisha herufi nyingi ipasavyo.<br><br>Anaacha nafasi inayofaa baina ya maneno. | Ana mwandiko usio nadhifu lakini unasomeka.<br><br>Anatenganisha baadhi ya herufi ipasavyo.<br><br>Anaacha nafasi zisizolingana baina ya maneno. | Ana mwandiko usiosomeka kwa urahisi.<br><br>Hatenganishi herufi nyingi ipasavyo.<br><br>Anaacha nafasi nyingi zisizolingana baina ya maneno. |
| Msamiati | Ana uteuzi mzuri wa maneno na matumizi anuwai ya | Ana uteuzi mzuri wa msamiati | Anatumia msamiati finyu ambao wakati | Anatumia msamiati finyu ambao haulingani na muktadha. |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | msamiati kulingana na muktadha. | uliotumika kulingana na muktadha. | mwingi haulingani na muktadha. | |
| Mpangilio (Muundo na mtindo) | Ana uwiano na mpangilio wa kipekee wa mawazo kuanzia mwanzo hadi mwisho.<br>Muundo na mtindo wa barua ya kirafiki umedhihirika.<br>Amebainisha utangulizi, mwili na hitimisho vilivyo.<br>Anaendeleza mawazo vizuri. | Ana mtiririko wenye mantiki.<br>Kuna uwiano na mfululizo wa mawazo.<br>Kuna utangulizi, mwili na hitimisho.<br>Anaendeleza mawazo vizuri. | Anajaribu kupanga mawazo kimantiki.<br>Utangulizi, mwili na hitimisho hujitokeza kwa kiasi.<br>Anaendeleza baadhi ya mawazo vizuri. | Hana mpangilio unaoeleweka wa mawazo na ni vigumu kufuatilia kazi yake. |

**SEHEMU C: FASIHI**

29. **ZOEZI 6: Fasihi Simulizi**

**a. Aina ya wimbo** **(alama 1)**

i. Bembelezi/ Bembea/ Pembejezi

b. **Sifa za wimbo wa aina hii** **(alama 2)**

i. Kumuongoa mtoto alale
ii. Urudiaji wa maneno na sauti.
iii. Kusihi/ kubembeleza.
iv. Kutoa ahadi ya vitu vizuri/ vya kufurahsha/ zawadi kwa mtoto
v. Unaimbwa na mlezi

c. Ukulima/ biashara ya bidhaa za kilimo **(alama 1)**

d. Mwenye kujali maslahi- anasema mtoto anamtia uchungu. Anasema atakula kidizi kimoja na mtoto viwili
Mwenye matumaini- Anampa mtoto matumaini kwamba mama atakuja
**(alama 2)**

e. **Mbinu za uwasilishaji wa wimbo darasani:**

- Kuimba kwa mtindo taratibu na sauti ya chini
- Kurudia sauti na maneno na vifungu ili wapate taathira ifaayo.
- Kuchezesha viungo vya mwili kulingana na ujumbe.
- Kutumia ishara zifaazo za uso kulingana na ujumbe
- Kuishirikisha hadhira katika kurudia baadhi ya sehemu au hata kupiga makofi.
- Kuvaa maleba/ mavazi yanyovalimwa na mlezi.

- Kupandisha na kushusha sauti kulingana na ujumbe.

**(Hoja 4x1 = 4 )**

30. **ZOEZI 7: NOVELA**

a) Aina mandhari

**Mahali:**

- Shuleni
- Nyumbani/sebuleni
- Jamii ya Tesi

**Wakati:**

Kipindi- wakati Tesi akiwa Gredi ya 7

**Hoja 2 x 1= 2**

**b) Uwajibikaji**

i. Tesi kuwaongoza wenzake kubuni kikundi cha Tufaane.
ii. Mwalimu kuwaelekeza wanafunzi kwenye mradi.
iii. Kikundi cha Tufaane kuilisha jamii kwa mboga.

**Hoja 1 x 1= 1**

**c) Masuala mengine**

a) Bidii - ya Tesi shuleni
b) Mshikamano- Tesi na wenzake,
c) Utu / ukarimu Kikundi cha Tufaane kuwasaidia wenye mahitaji
d) Elimu - Kikundi cha Tufaane kuwasaidia wenye mahitaji
e) Uwekezaji - Kuanzisha mradi wa kupanda mboga
f) Ukuzaji wa vipawa- Tesi alitambuliwa.
g) Teknolojia- video

**Hoja 3 x 1= 3**

d) Tesi ni mnyenyekevu. **(alama 1)**

**e) Mbinu za lugha za kuwasilisha ujumbe:**

i. **Tashibihi**-wafuasi wengi kama mchanga, bahati kama mtende, sifa zao kuenea kama moto nyikani
ii. **Urudiaji/ usambamba**- Si mchicha, si kabeji, si sukumawiki, si munavu hata mchunga na kisamvu zilikuwako.
iii. **Kidokezo cha methali** kuchanika kwenye mpini
iv. **Chuku**- wafuasi wengi kama mchanga wa bahari
v. **Nahau**-kupungia shule mkono, hakujitanua kifua, atajifunga kibwebwe
vi. **Taswira**- wafuasi ni wengi kama mchanga. Tunapata picha mawazoni.

**Hoja 3 x 1= 3**

## MIPAKA YA KUTUZIA SEHEMU (B)

## ZOEZI 3: UFAHAMU WA KUSOMA (READING COMPREHENSION)

| UPEO/ALAMA (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 10-12 | 4 |
| 7-9 | 3 |
| 4-6 | 2 |
| 1-3 | 1 |

## ZOEZI 4: SARUFI (GRAMMAR)

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 14-18 | 4 |
| 9-13 | 3 |
| 5-8 | 2 |
| 1-4 | 1 |

## ZOEZI 5: KUANDIKA (Alama 10)

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

## ZOEZI 6: FASIHI SIMULIZI (Alama 10)

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

## ZOEZI 7: NOVELA (Alama 10)

| UPEO (SCOPE) | KIWANGO CHA UTENDAJI (PERFORMANCE LEVELS) |
|---|---|
| 8-10 | 4 |
| 5-7 | 3 |
| 3-4 | 2 |
| 1-2 | 1 |

# KISWAHILI GRADE 7 ASSESSMENT SHEET: SEHEMU B naC

**(Tumia vigezo vya kutathminia ili kurekodi kiwango cha utendaji cha mwanafunzi: 4, 3, 2 ama 1)**

| S/NO | JINA LA MWANAFUNZI | ZOEZI 3 UFAHAMU WA KUSOMA | | | | ZOEZI 4 SARUFI | | | | ZOEZI 5 KUANDIKA | | | | ZOEZI 6 FASIHI SIMULIZI | | | | ZOEZI 7 NOVELA | | | | MAONI KUHUSU UTENDAJI |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **JINA LA MWANAFUNZI** | **4** | **3** | **2** | **1** | **4** | **3** | **2** | **1** | **4** | **3** | **2** | **1** | 4 | 3 | 2 | 1 | 4 | 3 | 2 | 1 | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |
| | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | | |